

HABARI FUPI



**Kumbukumbu ya Fr. Sebastian**

Alhamisi tarehe 5 Septemba, Padri Sebastian Gathogo aliaga dunia. Alizaliwa tarehe 1 Aprili 1943, kijijini Kibura, Parokia ya Kimondo, Jimbo Kuu la Nyeri. Alipadrishiwa mwaka 1973 kule Roma, na Papa Paulo VI, katika Basilika Kuu la Mt. Petro. Baada ya kuhudumu kwa muda kule Italia, alirudi nchini Kenya, akifunza katika Seminari, tena akihudumu katika Parokia kadhaa. Kuanzia Februari 2009 hadi Februari 2014 alihudumia Parokia yetu kama msaidizi wa Baba Paroko. Kisha akatumwa kule Tabor Hill, Nyahururu, alipofanya kazi hadi siku ya kufariki. Ibadia ya mazishi iliadhimishwa kule Mathari, Nyeri, na Askofu Mkuu Muheria, pamoja na Askofu wa Nyahururu Joseph Mbatia na Mapadri wengi. Wakristu wa Ol Moran wanamkumbuka Fr. Sebastian kwa upendo na moyo wa shukrani. Tumwembe ajaliwe na Mungu amani ya milele katika Kristu Mwokozi.



**Talanta za PMC**

Watoto wa PMC walishindana katika Talent Show ya kiparokia Jumamosi 9 Novemba, Ol Moran. Hivi karibuni, wataanza mipango ya mwezi wa Desemba na Novena ya Noeli.

**Nadhiri za CA**

Wanachama wa CA walifanya siku ya maombi ya kujitayarisha kwa Nadhiri Jumatano 6 Novemba, kule Githima. Jumapili 24 Novemba, Sherehe ya Kristu Mfalme, watafanya upya Nadhiri zao za CA katika ibada ya Misa ya saa tano, Ol Moran.

**Uteuzi wa Makatekista**

Bw. James Kamugwi alitoka katika Kanisa la Mbombo, akateuliwa Katekista Mkuu wa Minjore. Bw. Simon Kihethu aliteuliwa Katekista Mkuu wa Gitumba, akatoka Minjore. Bw. Peterson Muthua akaondoka Ngare Narok, akateuliwa Katekista Mkuu wa Mbombo, akisaidiwa na bi. Susan Wamaita, aliyetoka Gitumba.

**Semina za IRP 2019**

Mpango wa IRP (Initiation & Rites of Passage) umerudi. Ni nafasi ya pekee ya kuwaelimisha Kikristu wavulana waliomaliza KCPE na watakaotahiriwa, pia wasichana wa umri huo. Semina hizi zitasimamiwa na walimu wa Tumaini Academy, na zimeandaliwa kwa ajili ya watoto wote wanaotaka kupata masomo. Utaratibu ni kama ufuatavyo:

WAVULANA

- Ijumaa 8—Jumapili 10 Novemba: Semina ya kuanzia (kule Tumaini Academy, Ngare Narok)
- Jumapili 10 Novemba: Tohara (Ol Moran Health Centre)
- Jumapili 10—Jumamosi 23 Novemba: Siku za mapumziko (Pastoral Centre, Ol Moran)
- Jumapili 24 Novemba: Misa na Sherehe ya Kutokea/Graduation (saa tano, Kanisani Ol Moran).

WASICHANA

- Alhamisi 21—Jumamosi 23 Novemba: Semina (Tumaini Academy, Ngare Narok)
- Jumapili 24 Novemba: Misa na Sherehe (saa tano, Ol Moran).

Kalenda ya Novemba 2019 MAIN ACTIVITIES AND SUNDAY GOSPELS	
<b>Jumamosi 9 Novemba</b>	→ 09.00am: Ol Moran, PMC Talent Show → 10.00am: Nyahururu, Sherehe ya Miaka 20 ya Saint Martin CSA
<b>Jumapili 10 Novemba</b> - ya 32 ya Mwaka (Lk 20:27.34-38)	→ Misa - 7am: Ol Motunyi; 8am: Minjore; 9am: Githima; 10am: Mithuri; 11am: Ol Moran; 12noon: Mbombo (Baraka Day). → 05.00pm: Ol Moran, IRP: Tohara ya Wavulana
<b>Jumatano 13 Novemba</b>	→ 10.00am: Survey, Misa ya Kikundi cha Rafiki ya Siri
<b>Ijumaa 15 Novemba</b>	→ 03.00pm: Misa na Sherehe ya Uzinduzi wa PPC na PFC
<b>Jumamosi 16 Novemba</b>	→ 09.00am: Githima, Semina ya Kwaya → 09.00am: Mbombo, Misa na Sherehe ya Vijana wa Kanisa Dogo
<b>Jumapili 17 Novemba</b> - ya 33 ya Mwaka (Lk 21:5-19)	→ Misa - 7am: Survey; 9am: Miharati, Ngare Narok; 11am: Nagum, Ol Moran
<b>Alhamisi 21 Novemba</b>	→ 09.00am: Ngare Narok, IRP: Semina ya Wasichana (hadi Jumapili)
<b>Jumapili 24 Novemba</b> - Sherehe ya Kristu Mfalme (Lk 23:35-43)	→ Misa - 7am: Kabati; 9am: Kahuho (Sherehe ya Kanisa Dogo); 11am: Ol Moran (IRP Graduation)
<b>Jumamosi 30 Novemba</b>	→ 10.00am: Ngare Narok, Sherehe ya Kwaya
<b>Jumapili 1 Desemba</b> - ya 1 ya Majilio (Lk 23:35-43)	→ Misa - 9am: Magadi, Lounyek; 11am: Dam Mbili, Ol Moran; 12.30pm: Ndunyuriwo. → 04.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni
<b>Jumamosi 07 Desemba</b>	→ 10.00am: Ol Moran, Mkutano wa PARISH PASTORAL COUNCIL
<b>Jumapili 08 Desemba</b> —Sherehe ya Maria Imakulata	<b>Msimamizi wa Jimbo Katoliki la Nyahururu</b>

**SAUTI ya Mtakatifu MARKO**  
- No. 78, Year 11, Printed on 9<sup>th</sup> November 2019 - (NOT FOR SALE)  
SAINT MARK CATHOLIC PARISH - Ol Moran - Catholic Diocese of Nyahururu  
P.O.Box 20 - 20320 Kinamba - saintmark@olmoran.it - +254 720 924 153

Printed by POP-SIGNS MEDIA  
Nairobi - Tel. 0720 845 699 and 0724 236 271

Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Kisha aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Akawa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.



Gazeti la Parokia Katoliki ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran

N. 78 — Mwaka wa 11

Oktoba-Novemba 2019

# SAUTI ya Mtakatifu MARKO

KCCB Anti-Corruption Campaign: "Tuuvunje Mnyororo wa Ufisadi"

## Kanisa lapaza sauti kupinga ufisadi

Maaskofu wa Kenya walitangaza watu iweze kubadilika. Vema wame-miezi sita ya Kampeni Kupinga Ufisadi fanya Maaskofu: tendo lao limesaidia nchini Kenya, walipokuwa pamoja kule Subukia, siku ya Maombi ya Kitaifa, Jumamosi 5 Oktoba. Ma-amuzi yao yatokana na ukweli kwamba wananchi wameangamizwa sana na ufisadi. Papa Fransisko, katika ziara yake hapa Kenya Novemba 2015, alitangaza hivyo tu: "Ufisadi ni njia ya mauti. Ufisadi ni tamu kama sukari, lakini huduru kama ugonjwa. Ni sumu inayoharibu nchi!" Baada ya miaka minne, tunaona maana ya ujumbe ule. Maaskofu walitoa tamko rasmi (taz. The Echo), tena siku hiyo ya maombi wakatembea bila viatu mpaka altare, wakaapa na kutia sahihi kama ishara ya kujitolea kwao kupinga ufisadi. Hata hivyo, mimi naona hatari: ikiwa tendo hili litabaki tamko tu, halitatusaidia. Kupinga ufisadi, bila shaka, si kutangaza maneno, bali zinahitajika elimu na masomo, ili akili na mioyo ya

na mahubiri yetu. Tunahitaji elimu, si maonyesho pekee. Lazima tupange masomo hata kwe-tu: acha kuitisha wala kutoa "kitu kido-go", tushike haki, tusafishe jamii. Fr. Giacomo Basso - Baba Paroko

na mahubiri yetu. Tunahitaji elimu, si maonyesho pekee. Lazima tupange masomo hata kwe-tu: acha kuitisha wala kutoa "kitu kido-go", tushike haki, tusafishe jamii. Fr. Giacomo Basso - Baba Paroko

Maaskofu wakisoma tamko rasmi na wakiapa kupinga ufisadi.



Maaskofu wakisoma tamko rasmi na wakiapa kupinga ufisadi. Maaskofu wakisoma tamko rasmi na wakiapa kupinga ufisadi. Maaskofu wakisoma tamko rasmi na wakiapa kupinga ufisadi.

Natumaini ku-wa vita vya kupinga ufisadi visibaki muun-gamo kanisani au kuvaa ribon, bali iweze kuwa mpango wa ma-somo ya maana katika Makani-sa, Jumuiya, hadi shule zetu



**UZINDUZI WA HALMASHAURI ZA PAROKIA**

Kazi ya Uchaguzi 2019 katika Parokia imekamilika. Tulianza mwezi wa saba na Semina katika Makenisa, na uchaguzi wa Kamati za Makenisa Madogo, za Jumuiya Ndogo Ndogo na Zones. Kisha, Halmashauri Kuu za Parokia zimeveza kuundwa pia.

Ijumaa 11 Oktoba wanachama wa Parish Pastoral Council (PPC) wali-kutana mara ya kwanza, wakachagua Kamati Kuu, yaani Parish Executive Committee, pia wakachagua wanachama wa Parish Finance Council (PFC). PFC ilikutana Jumatatu 28 Oktoba, wanachama wakachaguana viti na majukumu.

Sasa Halmashauri ziko tayari kuanzisha huduma zao. Kutakuwa na Misa na Sala kwa Robo Mtakatifu, na Sherehe ya Uzinduzi wa PPC na PFC pamoja, Ijumaa 15 Novemba, kuanzia saa tisa, Ol Moran.

Baadaye, mkutano wa kwanza wa PPC utafanywa Jumamosi 7 desemba 2019, Ol Moran, saa nne asubuhi.

**KRISTU MFALME, MAJILIO, IMAKULATA.**

Baada ya Sherehe ya Watakatifu wote (1 Novemba) na Siku ya Kumbukumbu ya Waumini Marehemu wote (2 Novemba), siku muhimu ijayo katika utaratibu wa Kanisa itakuwa Sherehe ya Bwana Wetu Yesu Kristu Mfalme wa Ulimwengu (Christ the King). Itakuwa Jumapili 24 Novemba, iliyo Jumapili ya mwisho wa Kipindi "Cha Mwaka". Jumapili itakayofuata, tarehe 1 Desemba, itakuwa Mwanzo wa Mwaka Mpya wa Kiliturjia na Jumapili ya 1 ya Majilio, yaani Kipindi cha ku-jiandaa kwa Sherehe ya Kuzaliwa Mwokozi (Krismasi).

Sikukuu nyingine ya kukumbuka itakuwa tarehe 8 Desemba, Jumapili, iliyo Sherehe ya Maria Mkingina Dhambi ya Asili (Maria Imakulata), aliye Msimamizi wa Jimbo letu la Nyahururu.

## Mpango wa kuongezea miti kwenye Mkanisa na eneo Miti ya Kumbukumbu

Parokia imeanza mpangilio wa kuendeleza kazi ya kupanda miti katika Mkanisa yetu, kama vile kwenye eneo. Halmashauri Kuu imeamua kwamba kila wakati kutakapokuwa na Ubatizo katika Mkanisa yetu, kila atakayebatizwa atapewa mti wa kumbukumbu, atakaoupanda nyumbani. Tena, kila wakati itakapofanywa Baraka ya familia Kanisani (Baraka Day), kila familia itakayobarikiwa itapewa mche wa kupanda kwenye shamba la Kanisa, kama kumbukumbu pia. Mpango huu umeshaanza Ol Moran, Jumapili 20 Oktoba, wakati wa Ubatizo wa wanafunzi wa Tumaini Academy. Tena, siku ya Baraka kanisani Kabati na Mithuri, Jumapili 27 Oktoba, na Mbombo, Jumapili 10 Novemba.



Isitoshe, Parokia imekuwa na kazi ya kuongezea miti katika mashamba yake. Mwezi wa Oktoba miti zaidi ya 1,500 imepandwa kwenye shamba kuu, pia kwenye Gathanji Agroforestry, Ol Motunyi Agroforestry, Tumaini Academy, St. Stephen's Residence. Miti imeleta pia faida kwa Parokia yenyewe, katika kutafuta kuni na mbaao, tukikata miti iliyokauka au kupogolewa. Hata zaidi, miti huleta faida kwa mazingira na jamii ya eneo: tukikubali ukweli huu tutaishi vema zaidi.



## Fr. Sandro na Fr. Mariano warudi Italia Mapadri Wapya Jimboni

Siku iliyoadhimisha mambo makubwa katika Jimbo la Nyahuru ilikuwa Jumamosi 19 Oktoba. Baba Askofu aliongoza Ibada ya Misa kule Tabor Hill, pamoja na Mapadri na Wakristu wengi wa Jimbo la Nyahuru. Sababu za ibada hiyo zilikuwa kadhaa: HATIMA YA MWAKA WA UMISHIONARI - Mwaka wa Uenezaji wa Injili 2019 (Year of Mission) umefungwa rasmi, lakini Askofu aliwaalika wote kuendelea kufanya kazi kwa bidii katika kueneza Injili kwenye maeneo yetu.

MAPADRI WAPYA - Siku hiyo Mashemasi watatu walipadrishwa, ndiyo baraka kubwa kwa ajili ya Jimbo. Hao ndio Fr. David Gichinga, kutoka Parokia ya Mukeu; Fr. Joseph Nyaga Njuguna kutoka Mutanga; na Fr. Stephen Chege Ndegwa, kutoka Murungaru. Hivi karibuni watatumwa katika huduma zao.

KWAHERI KWA MAPADRI WA PADUA - Mwishoni mwa Ibada, Askofu aliwaaga Mapadri Wamishionari wa Jimbo la Padua, waliomaliza huduma yao Nyahuru na mwezi wa Desemba watarudi Italia: Fr. Mariano Dal Ponte, aliyekuja Kenya mwaka 2002, akahudumia Ol Joro Orok, Maina na St. Martin; pia Fr. Sandro Ferretto, aliyekuja nchini 2007, alihudumia Dundori na Mochongoi.

KUPINGA UFISADI - Kisha, Askofu Joseph alitangaza rasmi mwanzo wa Kampeni ya Kupinga Ufisadi, ilivyopangwa na Maaskofu Wakatoliki wa Kenya, kwa muda ya miezi sita ijayo (taz. uk. 1 na The Echo).

Chini: Baada ya Sherehe ya Jimbo, Fr. Sandro na Fr. Mariano waliagana na Wakristu wa Mochongoi, Jumapili 27 Oktoba. Baaada ya Ibada, walipewa alama za wazee Wakalenjin na Wakikuyu.



## Mashindano ya Jimbo Ushindi wa Kwaya ya Parokia

Wanakwaya wetu wamejaribu sana! Katika mashindano ya Jimbo la Nyahuru, kule Manunga, Jumamosi 12 Oktoba, waliweza kupata matokeo ya maana kati ya Kwaya 20 za Parokia mbalimbali: Folk Song: position 1; Set Piece II: position 2; Set Piece I: position 3; Own Composition: position 3; Over-All: Position 2.

Wanakwaya watasherehekea matokeo haya na kufunga mwaka Jumamosi 30 Novemba, wakikutana Ngare Narok, Tumaini Academy. Kesho yake, Jumapili 1 Desemba, ya kwanza ya Majilio, watakuwa na Ibada ya Shukrani Kanisani Ol Moran, saa tano.



SSP: Ufadhili wa Shule

## Madarasa ya Nagum

Mradi wa Ufadhili wa Shule (SSP, yaani School Support Program) umeanza kazi katika shule ya Nagum, kujenga angalau madarasa mawili mapya ya matope, jiko, na ukarabati wa madarasa mengine. Pia, umepeana viti kadhaa vya shule. Kwa kweli, hali ya mijengo ya Nagum ni mbaya zaidi. Parokia, iliyo mfadhili rasmi wa shule, imeamua kuchangia kiasi maendeleo yake. Ijapokuwa Shule ya Nagum (Laikipia West) ni ya Serikali, haijapata msaada wowote kwa ajili ya ujenzi mwaka huu wala mwaka uliopita. Vile vile, Shule za Dam Mbili na Ndunuriwo (Laikipia North) zimekosa msaada wa maendeleo. Na vile maeneo haya yahitaji kuinua elimu!

Hali mbaya ya madarasa katika Shule ya Nagum: Juu: Darasa la Nursery; Chini: Darasa la tano.



## Hekima na Tumaini

### Mwisho wa Mwaka wa Shule

EDUCATION DAY - Jumamosi 7 Septemba Wanafunzi na walimu wa Tumaini Academy na Hekima House walisherehekea sikukuu ya Elimu (Education Day), kule Ngare Narok, wakifungua rasmi kisima kipya cha maji katika shule ya msingi wa Tumaini. Waliweza kuhudhuria sherehe hata viongozi wa Parokia, wanafunzi wa Shule za Upili za Ol Moran na Mithuri, na wageni kadhaa, hata wafadhili wa shirika la "Maisha Marefu", waliosaidia kujenga kisima.

MWISHO WA MWAKA - Wanafunzi wa Tumaini Academy walifunga shule Jumatano 23 Oktoba. Wanafunzi 33 wa darasa la nane wa Tumaini walimaliza mthani wa KCPE. Hata Wanafunzi wa Hekima House walirudi nyumbani baada ya kufunga shule, Jumatano 23 Oktoba. Wamebaki Watahiniwa wa KCSE, walioanza mthani wao juma lililopita. Parokia inawatakiya hawa kufaulu katika mthani, na wanafunzi wote wakati mwema wa likizo.

Kulia: Education Day na Uzinduzi wa kisima cha Tumaini Academy, Ngare Narok.

Chini kusoto: Wanafunzi wa Hekima katika sherehe ya kufunga Mwaka wa Shule.

Chini kulia: Watahiniwa wa KCPE 2019 wa Tumaini.



## Shughuli za Vijana

KESHA YA WATAKATIFU - Kama kila mwaka, Vijana wa Parokia walikutana katika Kesha ya Watakatifu Wote (All Saints Vigil), Alhamisi 31 Oktoba, na kuadhimisha Misa pamoja Ijumaa 1 Novemba kwa sababu ya Sherehe ya Watakatifu wote.

RETREAT MOCHONGOI - Kuanzia Jumatano 6 hadi Jumapili 10 Novemba, Vijana wa Ng'arua Deanery wamekuwa na Retreat, yaani maombi na masomo ya imani.

Jumamosi, walitembea kutoka Mochongoi mpaka Nyahuru, wakahudhuria sherehe ya kutimiza miaka 20 ya shirika la St. Martin.

CALENDAR 2020 - Ofisi ya Vijana ya Jimbo la Nyahuru imetengeneza Calendar 2020 ya Vijana. Inauzwa Ksh 100: faida yake itachangia hazina ya Vijana wa Jimbo. Calendar inauzwa hata Parokiani.

MAKANISA MADOGO - Vijana wa Mkanisa Madogo wanaendelea kufanya kazi zao pia. Jumamosi 26 Oktoba Vijana wa Mithuri walifanya Charitable Day, wakawatembelea watoto wa Magnificat, Ol Moran, wakiwasaidia na zawadi zao. Jumamosi 16 Novemba, Vijana wa Mbombo watakuwa na siku yao ya Revival.

Kulia: Mfano wa Youth Calendar 2020.

Kushoto: Vijana wa Mithuri wakipeana zawadi kwa watoto wa Magnificat.

